Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

# Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

DOI: https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v4i1.362
Volume: 04 Issue: 01 | April-2022|
Received: 29.03.2022; Accepted 03.04.2022; Published on 30.04. 2022 at www.editoncpublishing.org
Kwambai, M., *Editon Cons. J. Kiswahili.* Double –Blind Peer Reviewed Journal

# AMEZIDI IMEZIDI.

**Matthew Kwambai.**
**Chuo Kikuu cha Egerton, Kenya.**
**Email: kwambai09@yahoo.com**

## IKISIRI

Makala haya yamelenga kuangazia muundo wa kipekee wa tamthilia hii na kuona jinsi muundo huu unavyowezesha uwasilishaji wa ujumbe wake. Tamthilia ya *Amezidi* ina muundo ambao ni tofauti na tamthilia nyingi za Kiswahili zilizoandikwa wakati mmoja. Nadharia iliyotumiwa katika kazi hii ni ya umuundo ambao unasema kuwa kazi ya fasihi inakuwa na muundo Fulani ambao unahusisha fani ambazo zitaweza kutumika katika kuwasilisha ujumbe na hivyo maudhui huwa na uhusiano mkubwa sana na fani zitakazotumiwa kuyawasilisha. Utafiti huu ulikuwa wa kimaktaba, ambapo vitabu mbalimbali vilirejelewa huku yaliyomo katika tamthilia ya *Amezidi* yakihakikiwa. Matokeo yalidhihirisha kuwa Wahusika wawili na wa pekee ambao wanatekeleza majukumu yote katika tamthilia yote, mbinu kama vile uradidi na chuku zinatumiwa na wahusika hawa kuendeleza maudhui kama vile: umaskini, utegemeaji wa misaada na ndoto zisizoweza kutimizwa. Kutokana na haya yote inadhihirika kuwa tamthilia hii ya kukithiri mipaka ya uhalisia inakengeusha wahusika sawa na wasomaji wa tamthilia hii.

**Maneno muhimu:** Chuku, kithiri, muundo, uwasilishaji, ukengeushi.

-----***-----

**How to cite this article in APA.**
Kwambai, M. (2022). Amezidi Imezidi. *Editon Cons. J. Kiswahili,* 4(1), 427-433. https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v4i1.362

-----***-----



©2022, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non-Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

# Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

DOI: https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v4i1.362
ISSN: 2663-9289
Volume: 04 Issue: 01 | April-2022|
Received: 29.03.2022; Accepted 03.04.2022; Published on 30.04. 2022 at www.editoncpublishing.org
Kwambai, M., *Editon Cons. J. Kiswahili*. Double –Blind Peer Reviewed Journal

**UTANGULIZI**

Kazi ya *Amezidi* ina maonyesho mbalimbali ambayo yanafanyika mawazoni. Onyesho la kwanza linafanyika pangoni na kudhihirisha maisha duni ya Ame na Zidi. Uvivu wao unawafanya kulala kwa muda mrefu na kukaa kwa njaa huku wakiota mambo makubwa yasiyoweza kutimizika. Onyesho la pili linafanyika pangoni katika ndoto ya Ame na Zidi. Wanasema jinsi ambavyo wameagiza vitu mbalimbali vya kurembesha kasri lao kutoka nchi mbalimbali kama Paris na Iran. Onyesho la tatu linafanyika Pangoni na inahusisha Zidi na mpenzi wake Mari na ndoto ya Zidi pamoja na mambo ambayo hayawezekani yanamfanya Mari kughadhabishwa na Zidi. Onyesho la nne linafanyika mawazoni kwenye pango na linahusisha wanafunzi na mwalimu. Kuna maswali na majibu na mwalimu wakati mwingine anashindwa kujibu maswali na hivyo kuwaelekezea wanafunzi ambao wanajibu vyema. Onyesho la tano linafanyika mawazoni na pango linageuka ofisi na bosi na msaidizi wanaangazia jinsi wafanyakazi wanashindwa kufanya kazi kwa kuwa wanaelewa nadharia huku wakishindwa kuitekeleza. Pia wanapanga kuagiza vitu vingi ughaibuni huku wakiwa na azma ya kuiba pesa za umma. Onyesho la sita liko mawazoni kwenye pango, Ame na Zidi wanajadili ukaguzi wa ofisi wanapofanya kazi kuangazia pesa za umma zilizoibwa. Onyesho la saba linafanyika mawazoni mwa wahusika, Mari amekengeuka na hivyo kujipamba nywele na midomo, Zidi anamkaribisha huku akimpa ahadi ya vitu kutoka ngambo ambavyo viko mawazoni tu. Onyesho la nane liko pangoni kati ya Ame na Zidi, wanahisi njaa huku wakiwa hawana chakula ila misaada ambayo imeoza na hawana kitu cha kutumia kuwasha moto ili wapike. Onyesho la tisa, linafanyika mawazoni kwenye pango, Zidi na Ame wanapanga sherehe ya kuzaliwa kwa kutumia pesa maradufu ya zilizotumika mwaka uliotangulia huku wakiwa hawana pesa hata shilingi moja. Mwisho onyesho hili la tisa, Zidi anafariki kwa kuumwa na tumbo baada ya kula nyama ya msaada. Onyesho la kumi, linafanyika mawazoni, kwenye pango na Ame pia anaugua kwa kula nyama ya msaada, anaumwa na tumbo kabla ya kufariki. Kutokana na maelezo haya, utafiti huu uliangalia fani ilivyochangia kufafanua wahusika na kuendeleza maudhui katika tamthilia ya *Amezidi.*

**MAPITIO YA MAANDISHI**

Scholes (1974), anashikilia mawazo kwamba ni muhimu kutumia Umuundo katika uhakiki wa fasihi kwa sababu lugha na fasihi zina uhusiano mkubwa sana kwani fasihi hutumia lugha kama nyenzo ya kuyapitishia maudhui ya wasanii. Mhakiki wa kimuundo anapaswa kutambua vipengele mbalimbali vinavyoujenga mfumo unaotawala matumizi ya nadharia ya Umuundo na namna ya kuviunganisha (Jefferson & Robey 1986). Nadharia ya Umuundo husisitiza vipengele vya kazi ya sanaa, jinsi vinavyohusiana hadi kuikamilisha kazi ya fasihi. Nadharia hii haiangalii kila kipengele peke yake lakini huangalia mahusiano yaliyoko baina ya vipengele vyote. Vipengele huhusiana kama viunganisho vya mkufu na huamua uhusiano wao (Scholes, 1974; Wafula & Njogu, 2007).

**MATOKEO YA UTAFITI**

**Mbinu Zinazidhihirisha Kuzidi kwa *Amezidi***

*Amezidi* imetumia mbinu kama vile wimbo, chuku, uradidi na maswali ya balagha kuendeleza tamthilia. Wimbo wa kwanza unapatikana ukurasa wa 1-3 na unadhihirisha kutamauka kwa yule anayeimba, anasema kuwa amefanya mengi na hajapata faida yoyote na hivyo anangoja kaburi na anatuma salamu kwa waliofariki kabla yake na kuwaeleza kuwa siku zake zimefika na anaelekeo huko kuzimu karibuni. Wanafunzi wanaimba wimbo wa tajiri katika ukurasa wa 33-35, wimbo huu unaonyesha tamaa ya tajiri ambaye anakula kila kitu kiasi cha kumfanya alale na kukosa kufikiria, tajiri amemeza chuma, mafuta na vitu mbalimbali vya dhahabu na mwisho hajielewi, amelala akiwa amesimama na akiwa macho. Ame na Zidi wanaimba wimbo katika ukurasa wa 68, kuonyesha uvivu wao wa kulala kwa muda na hivyo miaka mingi imepita bila ya kutokea mabadiliko ila wako jinsi walivyokuwa miaka ya nyuma. Wimbo wa mwisho uko katika ukurasa wa 86-87,



©2022, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non-Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

# Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

DOI: https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v4i1.362
ISSN: 2663-9289
Volume: 04 Issue: 01 | April-2022|
Received: 29.03.2022; Accepted 03.04.2022; Published on 30.04. 2022 at www.editoncpublishing.org
Kwambai, M., *Editon Cons. J. Kiswahili.* *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

unaoangazia ndoto ya siku ambazo zitakuja. Wimbo huu unasema kuwa mwanzo utaanza utakapofika mwisho, kuwa waliofariki watafufuka na waliolala wataamka na kwamba mambo yaliyowalemea watayabeba na kuwa kutakuwa na mabadiliko. Kwa mujibu wa Diegner (2002).

*Rosa Mistika* ni fumbo la kudhihirisha kukosa kufanikiwa kwa suala la kukombolewa kwa mwanamke na binadamu kwa ujumla miaka ya 1960. Katika *Gamba la Nyoka,* anasema ni riwaya ngumu kuelewa kama fumbo, hata hivyo anasema kuwa maana ya ndani ya mada ya kitabu hiki ni kuvua ukale na kukubali mambo mapya yanayojumuisha kubadili mtazamo. Nyimbo zilotumika katika *Amezidi* ni mafumbo ya tamaa, upumbavu na matumaini ambayo hayatimiziki ya Waafrika.

Aidha, kuna mbinu ya chuku ambayo imetumika sana kutoka mwanzo mpaka mwisho wa tamthilia. Mambo mengi yanafanyika mawazoni na yanaangazia mambo makubwa ila yale yanayofanywa na Ame na Zidi ni mchezo wa kuota makubwa ambayo hayawezi kufanyika. Wanasema kuwa wao wanaishi kwa kasri na kuwa wana zulia, sofa na magari yaliyoletwa kutoka Paris na Iran. Chuku hii inasababisha kinaya kwa sababu wao wanalala kwa muda mrefu sana bila kujihusisha na kazi yoyote, wanakaa kwa majani ndani ya pango. Mambo haya yote yanadhihirisha uvivu wa hali ya juu kiasi cha Ame na Zidi kutegemea msaada wa nyama ambazo zimeoza. Kila kitu kwao kinaletwa kutoka ngambo, hata kiberiti ya kupikia mhogo na nyama walioletewa kama misaada ya E.C. na mwisho wanakula vyakula hivi mbichi na kufa kutokana na ugonjwa wa kipindupindu. Pia, wanapanga sherehe ya siku kuzaliwa kwa kualika watu wengi na kupanga kutumia pesa nyingi sana, mipango ni chuku ambayo iko akilini na wala haitimii kamwe.

Kuna mbinu ya uradidi ambao unatumiwa kutoka mwanzo mpaka mwisho, kila kauli inayosema na Ame inarudiwa na Zidi, hali hii inasisitiza uvivu na ujinga walio nao wahusika hawa wawili. Mmoja wao anapouliza swali, mwenzake anarudia swali lile huku akitaka mwenzake ajibu. Uradidi huu unaonyesha tamthilia yote kama mzaha ambao hauna suala zito. Mwalimu na mwanafunzi wanachezeana shere kupitia kwa kurudia maswali na kauli mbalinbali kiasi cha kwamba, mwalimu anaonekana kuwa hakuhitimu na anashindwa kujibu maswali ya mwanafunzi wake. Tamthilia inakuwa kama mchezo wa kujadili mambo yale yale na hakuna jambo zito. Hii inasababababisha hali ya kukithiri mipaka kwa tamthilia ya *Amezidi* na ndiposa utafiti huu unaona kuwa *Amezidi* imezidi.

Mbinu ya maswali balagha imetumika sana katika *Amezidi*, Ame anauliza swali kwa mwenzake Zidi naye Zidi anamrushia swali lile lile Ame. Bosi na Msaidizi wake pia wanatumia mbinu hii sawa na Mwalimu na mwanafunzi na Zidi na Mari. Hali hii inadhihirisha ujinga wa wahusika wa tamthilia hii sawa na mzaha mwingi ambao umekithiri mipaka. Maswali haya yanamsaidia msomaji wa tamthilia kutafakari kwa undani kiwango cha elimu na ujuzi walio nao wahusika katika kazi hii ya *Amezidi*, hasa mwalimu ambaye badala ya kujibu maswali ya wanafunzi yeye anawarejeshea na wanafunzi wanajibu maswali mpaka mwalimu anashangazwa. Hali kadhalika, maswali haya yanamtafakarisha msomaji kuangazia elimu ya mazingira ya kitabu cha *Amezidi* kuwa ni ya kinadharia tu na hivyo mfanyakazi akifika mahali pa kutekeleza mambo aliyofunza kwa kazi aliyojifunza anashindwa. Mbinu ya maswali ya balagha inakithiri mipaka na hivyo kuendeleza hali kuwa *Amezidi* imezidi. Sakkos (2008), anavyosema kuwa mada ya kitabu *Kichwamaji* ni fumbo la Waafrika kugengeuka kwa kutafuta elimu ya kimagharibi ili wapate kazi. Waafrika kama Ame na Zidi wamegengeuka na wanategemea wazungu ili wapate misaada mbalimbali ikiwemo ya vyakula.

**Kuzidi kwa Ame na Zidi**

Ame na Zidi ni wahusika wa kipekee. Wanadhihirisha sifa kama vile uvivu, uzembe na upumbavu unaopita mipaka. Hii



©2022, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non-Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

# Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

DOI: https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v4i1.362
ISSN: 2663-9289
Volume: 04 Issue: 01 | April-2022|
Received: 29.03.2022; Accepted 03.04.2022; Published on 30.04. 2022 at www.editoncpublishing.org
Kwambai, M., *Editon Cons. J. Kiswahili.* Double –Blind Peer Reviewed Journal

inaonyeshwa na hali kwamba, wanalala mpaka wanashindwa kutayarisha chakula cha msaada ambacho wanarushiwa kwa sababu ukame na njaa uliokabili nchi yao. Wahusika hawa wana sifa zinazofanana kiasi cha kutoweza kuwatofautisha. Wana sifa kama vile uvivu, uzembe na upumbavu. Wanalala kwa muda mrefu sana mpaka wanashindwa kutayarisha vyakula ambayo wameletewa kama misaada. Pia, wanashindwa kwenda kazini kwa muda mrefu sana na pale wanapopata fursa ya kwenda wanatunga uwongo kwamba walikuwa wagonjwa. Uzembe ambao wako nao unawafanya kuwa na ndoto zisizoweza kutimizwa, wanasema kuwa wanaishi katika kasri yenye vitu vingi kutoka nchi za nje, lakini ukweli ni kwamba wanaishi kwenye pango ambalo halina viti, zulia wala chakula. Mambo haya yanafanana na mawazo ya Lanfranchi (2012), ambaye anasema kuwa, licha ya Kezilahabi kupinga uhakiki wa fasihi kwa kuangazia mitazamo ya kimagharibi, uandishi wake unadhihirisha kuwa ameathiriwa na wanafalsafa wengi wa kimagharibi. Nchi za Kiafrika zinategemea nchi za Kimagharibi huku wakibakia kuiga utamaduni wa wazungu kikasuku na kuacha utamaduni wao. Ame na Zidi wanasema kuwa kila kitu chao kitaletwa kutoka ngambo kwa wazungu. Pale ambapo wanachukua jukumu la kuwa mwalimu na mwanafunzi, mwalimu anashindwa kujibu swali la mwanafunzi na mwisho anamuuliza mwanafunzi Swali Lake, mwanafunzi anajibu vizuri kushinda mwalimu. Pia, kwa upande wafanyakazi, wanasemekana kwamba walifunzwa na walikuwa wameshindwa kutekeleza nadharia kuwa matendo. Matukio haya yote yanaonyesha athari ya elimu ya kimagharibi ambayo inaendeleza ukoloni mambo leo, akili ya mwafrika inaongozwa na mawazo ya utegemeaji wa wazungu huku akishindwa kujitegemea na kutekelezwa mambo ambayo amesoma katika elimu hii ya kikoloni. Wahusika Ame na Zidi ni wapumbavu kama inavyodhihirika kupitia kwa maongezi yao ambayo yamejaa maswali ya balagha sawa na kila mmoja wao kurudia maongezi ya mwenzi wake badala ya kutoa majibu.

Jambo linalokithiri mipaka ukiangazia wahusika hawa ni kuwa wako katika dunia yao pekee, hawana jirani wala mtu mwingine wa kushiriki naye katika mambo mbalimbali. Wanatekeleza kazi ya kuwa bosi na msaidizi wake, mwalimu na mwanafunzi, Zidi na mpenzi wake, Mari. Haya ni majukumu mengi sana ambayo yanatekelezwa na wahusika hawa wawili, swali linaloibuka ni kuwa, katika mazingira ya uigizaji, wahusika wawili Ame na Zidi, wataweza kutekeleza majukumu haya yote ambayo wamepewa katika tamthilia ya *Amezidi*? Majukumu haya ambayo wamepewa yamepita mipaka, kwani katika tamthilia tunaona kwamba, Ame anabadilika na kuwa Mari ambaye ni mpenzi wake Zidi na bado tunasikia sauti ya Ame kwenye nyuma ya jukwaa ilhali alikuwa anaigiza kama Mari. Jambo hili haliwezi kufanyika kihalisia na hivyo kudhihirisha kuzidi na kupita mipaka ya kihalisia kwa tamthilia ya *Amezidi*.

Hali kadhalika, wahusika hawa wawili, Ame na Zidi, wako pekee yao katika mazingira yale ambayo wanaigiza na kuendeleza matukio, hawana ndugu, jirani na wala watoto. Suala hili ni la kushangaza mno, kwani binadamu hukua kwa kujumuika na watu wengine katika jamii. Wahusika hawa wawili wanaishi pekee yao, wanasema kuwa majirani na hata wanyama na kila kitu kingine kimemalizwa na ukame na wamebaki wao tu. Baadaye Zidi anafariki na kumwacha Ame pekee duniani. Mwisho Ame anafariki na kuacha dunia bila mtu, hili ni jambo ambalo linafanya usawiri wa wahusika kuweza kupita mipaka. Swali linaloibuka ni kuwa, je kuna uwezekakano wa watu wote kufariki na kuacha dunia bila mtu yeyote. Utafiti huu, ulibaini kuwa hali hii imekithiri mipaka na kuwafanya wahusika Ame na Zidi kuzidi sawa na matukio na mandhari yao kupita mipaka ya uhalisia.

Aidha, wahusika hawa wawili ni watu ambao wanaota tu bila ya kupata chochote kile katika maisha yao. Wanaota kununua viti, zulia na magari. Zidi ana ndoto ya kumnunulia Mari, vitu mbalimbali ya urembo, Mari anapomtembelea



©2022, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non-Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

DOI: https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v4i1.362
ISSN: 2663-9289
Volume: 04 Issue: 01 | April-2022|
Received: 29.03.2022; Accepted 03.04.2022; Published on 30.04. 2022 at www.editoncpublishing.org
Kwambai, M., *Editon Cons. J. Kiswahili.* Double –Blind Peer Reviewed Journal

anakasirika sana kuwa yote anayoelezwa ni ndoto wala si kitu cha kihalisia. Hali hii inamfanya kumwacha Zidi. Pia, Ame na Zidi, wanapanga sherehe ya siku ya kuzaliwa na kualika watu wengi sawa na kuwa na makadirio ya mamilioni ya pesa, ambayo wanasema ni mara mbili mwaka uliotangulia. Mambo haya yote ni ya kifantasia na hakuna hata mojawapo ambalo linatimizwa. Kilele cha kila kitu katika ndoto hizi zisizo na kikomo ni njaa na ugonjwa wa kipindupindu unaomwangamiza Zidi kwanza na kisha Ame. Kwa hivyo mambo yote ambayo ni maazimio ya Ame na Zidi ni masuala ambayo ni ya kufikirika na wala hakuna jambo hata moja ambalo linaweza kutimizwa. Haya yote yanapeleka mambo kwa dunia ya kufikirika bila kuweza kutimizwa na hivyo kuyafanywa kuzidi kama linavyodhirishwa na majina ya wahusika wawili Ame na Zidi na jina la kitabu *Amezidi*.

**Maudhui ambayo Yamezidi na Kupita Mipaka**

Kwanza kuna maudhui ya uvivu, Ame na Zidi ni wahusika wavivu sana. Wao wanalala kwa muda wa mwaka mzima. Hii inadhihirika kupitia mazungumzo yao. Hali hii imepita mipaka kwa sababu kazi kuu ambayo inaonekana kufurahikiwa na Ame na Zidi ni kulala kwa muda mrefu, wanalala mpaka wanashindwa kutayarisha chakula. Pia, kulala kwao kunawafanya kukosa kazi kwa muda mrefu sana mpaka wanapanga njama kwamba wakirudi kazini wataenda kueleza kuwa walikuwa wagonjwa. Wanapanga namna ya kwenda kwa daktari ili kupata stakabadhi itakayothibitisha kuwa kwa hakika walikuwa wagonjwa. Jambo la kushangaza katika uvivu wao ni kuwa wanashindwa kutoa maganda ya muhogo sawa na kuwasha moto wa kuchoma muhogo na nyama ya msaada, badala yake wanakula vyakula hivi bila ya kupikwa na mwisho wanapatwa na ugonjwa wa kipindupindu. Lanfranchi (2012), anasema Kezilahabi anazingatia kuwa lazima fasihi ya Kiafrika iweze kutoa uhuru kwa Waafrika. Hata hivyo Lanfranchi anasema kuwa, licha ya Kezilahabi kupinga uhakiki wa fasihi kwa kuangazia mitazamo ya kimagharibi, uandishi wake unadhihirisha kuwa ameathiriwa na wanafalsafa wengi wa kimagharibi. Sawa na mawazo haya, wahusika Ame na Zidi ambao wanawakilisha Waafrika wanategemea misaada kutoka kwa Wazungu, hawawezi kufikiria masuala yanayowahusu Waafrika, kila kitu kinafaa kutoka ngambo. Waafrika wamekegeuka kiasi cha kuona kuwa kila kitu bora kinatoka kwa Wazungu.

Kuna utemeaji wa msaada na umaskini uliokithiri mipaka. Wahusika wawili wakuu ambao hawafanyi kazi ila kuota kuwa wameleta vitu vingi kutoka kwa Paris na Iran wanajitokeza kutoka mwanzo mpaka mwisho wa *Amezidi*. Wanalala bila kufanya kazi na hata ikifika kwa kuwasha moto wanategemea kiberiti ambayo inaagizwa kutoka ngambo. Huu ni utegemeaji unaowafanya wahisika Zidi na Ame watumwa wa kuota na kungoja msaada kutoka kwa E.C. wanatemea misaada kwa kila kitu, kazi yao ni kulala na kungoja chakula kutupwa kutoka angani. Umaskini unadhihirika kupitia kwa nguo zilizochanika. Matokeo ya kutegemea misaada ni kuwa, Ame na Zidi wanangojea sana mpaka njaa inaanza kuwadhuru huku wakipata misaada hiyo dakika zao za mwishomwisho katika baa lao la njaa. Badala ya misaada kuwafaa na kuwasaidia, inakuwa chanzo ya vifo vyao. Inawaletea kipindupindu na mwisho kifo, kinachohitimisha maisha yao ya umaskini na uzembe mwingi. Misaada wanayongoja inakuwa chambo cha kuwaletea magonjwa sawa na vifo vinavyowamaliza na kuwatoa katika dunia ya shida nyingi. Misaada inawakengeusha Ame na Zidi na kuwafanya kutegemea misaada sawa Sakkos (2008), anavyosema kuwa mada ya kitabu *Kichwamaji* ni fumbo ya Waafrika kugengeuka kwa kutafuta elimu ya kimagharibi ili wapate kazi. Hali hii inawakengeusha na kuwatenga na utamaduni wa Kiafrika sawa na inavyodhihirika katika Amezidi, Ame na Zidi wanategemea misaada kutoka kwa wazungu.

Ujinga na upumbavu ni madhui mengine muhimu, wahusika wakuu katika tamthilia ya *Amezidi* wanaonekana kuwa wajinga na wapumbavu kupita mipaka. Jambo kuu



©2022, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non-Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

DOI: https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v4i1.362
ISSN: 2663-9289
Volume: 04 Issue: 01 | April-2022|
Received: 29.03.2022; Accepted 03.04.2022; Published on 30.04. 2022 at www.editoncpublishing.org
Kwambai, M., *Editon Cons. J. Kiswahili.* Double –Blind Peer Reviewed Journal

wanalofanya ni kuulizana maswali na kurudia yale mwenzi anasema bila ya kutoa jibu au maelezo. Hali hii inadhihirika katika miktadha ya darasani, na kazini kwa wafanyakazi. Kwa kuzingatia mwalimu darasani, analemewa na maswali ya mwanafunzi, anamuuliza mwanafunzi swali lake na mwanafunzi analijibu vizuri sana. Hii ni kejeli ya hali ya juu kwa walimu ambao wanafaa kuelewa masuala ili wafundishe wanafunzi na jamii kwa ujumla. Kwa upande wa wafanyakazi wanaonyeshwa kuwa wajinga na wapumbavu kwa kutoweza kutekeleza mambo waliofunza katika kusomea kazi mbalimbali. Wamitila (1998), anatafiti kazi za Kezilahabi *Rosa Mistika, Kichwamaji, Gamba la Nyoka, Dunia Uwanja wa Fujo, Nagona* na *Mzingile* na kudhihirisha kuwa dunia ni mahali pabaya na hivyo binadamu anafaa kuishi leo na hasijihusishe na masuala ya kesho. Ame na Zidi wametamauka na badala ya kusuluhisha matatizo wanakuwa na matumaini yasiyoweza kutimika.

Maudhui ya maisha ya ndoto na kukosa kutekeleza nadharia ya masomo yao, yanaranda katika tamthilia ya *Amezidi*. Kuna mambo ambayo yako tu kwenye ndoto na hayawezi kutekelezwa. Wahusika Ame na Zidi, mwalimu na wanafunzi na bosi na msaidizi wake wanadhihirisha ndoto na maisha ya kufikirika tu bila kuweza kutekelezwa. Vitu vingi kama zulia na viti vimeagizwa kutoka Paris na Iran, lakini ukweli ni kwamba wahusika Zidi na Ame wanaishi kwa umaskini usiomithilika, wako kwenye pango na waketi kwenye majani. Pia, wanapanga sherehe ya siku ya kuzaliwa na makaridio ni mamilioni ya pesa huku wageni wakiwa maradufu mwaka uliotangulia. Baada ya haya yote, wahusika hawa wanashindwa kupata pesa za sherehe hizi kwa sababu ya umaskini. Masomo ya wafanyakazi ni kitu ambacho hakiwasaidii, wao wanaelewa masuala kinadharia lakini hawawezi kutekeleza mengi ya masuala waliojifunza walipokuwa wakisomea kazi. Mambo haya yote yanapeleka maisha katika mandhari ya tamthilia ya *Amezidi* katika ulimwengu wa fantasia, ndoto na ya kufikirika. Kila kitu kinasubiriwa bila ya kutimizika huku wahusika wakiwa katika umaskini usiokuwa na kifani. Wao ni maskini hohe hahe, hawana mbele wala nyuma, Ame na Zidi wanaweka mawazo yao kuwa wanaishi kwa kasri, lakini wako kwenye pango na wanategemea vyakula vya misaada. Maisha yao ni ya uchochole, mwisho wanakula chakula cha msaada kinachowasababishia ugonjwa wa kipindupindu na hatimaye kifo. Haya yote yanathibitisha kuwa tamthilia ya *Amezidi* Imezidi.

Kwa ujumla, uchunguzi huu umedhihirisha kuwa, kila kitu katika tamthilia ya *Amezidi* kimekithiri mipaka na kuingia katika ulimwengu wa kufikirika na hivyo kukosa kuwakilisha masuala katika jamii, badala yake jukumu kuu linalotekelezwa na fantasia hii ni kukejeli na kudhihaki mambo ambayo yanafanyika katika jamii. Masuala ya elimu, uvivu kazini, wizi wa mali ya umma pamoja na utegemeaji wa misaada imedhihakiwa kwa mapana na marefu. Diegner (2002), anangazia mafumbo katika mada ya vitabu vinne vya Kezilahabi alivyotafiti: *Rosa Mistika, Kichwa maji, Dunia Uwanja wa Fujo* na *Gamba la Nyoka.* Anasema *Rosa Mistika* ni fumbo la kudhihirisha kukosa kufanikiwa kwa suala la kukombolewa kwa mwanamke na binadamu kwa ujumla miaka ya 1960. Katika *Gamba la Nyoka,* anasema ni riwaya ngumu kuelewa kama fumbo, hata hivyo anasema kuwa maana ya ndani ya mada ya kitabu hiki ni kuvua ukale na kukubali mambo mapya yanayojumuisha kubadili mtazamo. *Amezidi* ina maana ya ndani kuwa Waafrika ni watu ambao si huru ila wanaendelea kuongozwa kupitia misaada na uagizaji wa vitu kutoka nchi za ughaibuni.

## MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO

*Amezidi* imetumia wahusika wawili pekee ambao wanatekeleza majukumu yote katika tamthilia yote, mbinu kama vile uradidi na chuku zinatumiwa na wahusika hawa kuendeleza maudhui kama vile: umaskini, utegemeaji wa misaada na ndoto zisizoweza kutimizwa. Kutokana na haya yote inadhihirika kuwa tamthilia hii ya kukithiri mipaka, hivyo *Amezidi* imezidi.



©2022, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non-Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

**Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)**

**ISSN: 2663-9289**

**DOI:** https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v4i1.362
**Volume: 04 Issue: 01 | April-2022|**
**Received: 29.03.2022; Accepted 03.04.2022; Published on 30.04. 2022 at** www.editoncpublishing.org
**Kwambai, M., *Editon Cons. J. Kiswahili.* *Double –Blind Peer Reviewed Journal***

**MAREJELEO**

Diegner, L. (2002). Allegories in Euphrase Kezilahabi's Early novels. In: *Swahili Forum* 9, 43-74.
Jefferson, A., & Robey, D. (1986) *Modern Literary Theory* Batsford Ltd.
Lanfranchi, B. (2012). Daring to Be Destructive Euphrase Kezilahabi's Onto-Criticism. *Swahili Forum* 19, 72-87.
Sakkos, T. (2008). Existentialism and Feminism in Kezilahabi's Novel *Kichwamaji, Swahili Forum* 15, 51-61.
Scholes, R. (1974). *Structuralism: An Introduction*. Yale University Press New Haven.
Wafula, R., & Njogu, K (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Jomo Kenyatta Foundation.
Wamitila, K. (1998). A Philosophical Labyrinth: Tracing Two Critical Motifs in Kezilahabi's Prose Works. *AAP* 55, 79-91.



**©2022, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non-Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website:** www.editoncpublishing.org